

**HOTUBA YA KATIBU MKUU, WIZARA YA FEDHA  
NA MIPANGO, BW. DOTO M. JAMES WAKATI WA  
HAFLA YA KUSAINI NA BENKI YA MAENDELEO YA  
AFRIKA, MIKATABA MIWILI YA MIKOPO YENYE  
THAMANI YA SHILINGI BILIONI 589.26 KWA AJILI  
YA UJENZI WA BARABARA YA KABINGO-KASULU-  
MANYOVU (KM 260) KWA KIWANGO CHA LAMI,  
TAREHE 05 MACHI, 2019 KATIKA UKUMBI WA  
HAZINA, DAR ES SALAAM**

*Dkt. Alex Mubiru, Mwakilishi Mkazi wa Benki ya  
Maendeleo ya Afrika,*

**Mwakilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,**

**Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara,**

**Mwakilishi wa Taasisi ya Kusaidia Usafiri Kanda ya  
Kati (Central Transport Corridor),**

**Maafisa wa Serikali,**

**Wageni Waalikwa,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Habari za asubuhi!**

1. **Ndugu Mwakilishi Mkazi**, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kutumia fursa hii kuelezea furaha tuliyonayo ya kuweza kusaini na wewe, Mikataba miwili ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika itaipatia Serikali ya Tanzania mikopo yenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 256.2 (takribani shilingi bilioni 589.26)** kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Kabingo-Kasulu-Manyovu (KM 260)** kwa **Kiwango** cha lami na Uboreshaji wa Miundombinu ya Huduma za Jamii. Ninapenda kutoa shukrani za dhati za Serikali kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za uwekezaji katika miundombinu ya usafiri. Benki hii imekuwa mshirika wa muda mrefu wa Serikali katika maendeleo ya miundombinu na uwekezaji umekuwa wenye ufanisi na matokeo ya kuridhisha.
2. **Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**, utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano, ambao unalenga katika uimarishaji wa miundombinu ya usafiri ili kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupunguza umaskini na kuimarisha ushirikiano wa kikanda. Barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu ni kiunganishi muhimu katika maendeleo na uboreshaji

wa biashara ndani na nje ya nchi. Mradi wa ujenzi wa barabara hii utakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya Rumonge - Gitaza (km-45) nchini Burundi ili kuboresha mtandao wa barabara za Afrika Mashariki.

3. **Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**, mradi wa ujenzi wa barabara hii utakapokamilika utaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na mikoa ya magharibi mwa Tanzania na kufungua masoko ya kikanda nchini Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, mradi utachangia katika; (i) kupunguza gharama za uendeshaji magari na kuboresha usalama wa barabara; (ii) kupunguza gharama zingine za usafirishaji (logistical costs); na (iii) uboreshaji wa upatikanaji wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi kwenye maeneo ya mradi mkoani Kigoma.
4. **Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**, mradi huu unahusisha (i) ujenzi wa barabara ya Kabingo-Kasulu-Manyovu (km 260); (ii) Kuboresha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kufikie hadhi ya kituo cha umahili wa usalama barabarani katika kanda ya Afrika Mashariki (regional centre of excellent for road safety); (iii) Ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha

Forodha(One Stop Border Post) katika Mpaka wa Manyovu (Tanzania) / Mugina (Burundi), na (iv) uboreshaji wa miundombinu ya huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na: ukarabati wa masoko katika maeneo ya Makere na Manyovu; Usambazaji wa maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya Busunzu, Kasulu, Buhigwe na Manyovu; ujenzi wa vituo vya afya huko Makere na Busunzu, na ukarabati wa hospitali katika wilaya za Kasulu na Kibondo, pamoja na ujenzi wa kilomita 1 ya barabara ili kuzifikia huduma hizi za jamii.

5. **Ndugu Mwakilishi Mkazi**, natambua kwamba maandalizi ya nyaraka na hatimaye kusainiwa kwa mikataba ya mkopo za ufadhili wa mradi huu hivi leo imehusisha wadau wengi na muda mrefu wa kazi nzito na kujitoa katika kufanikisha. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kibinafsi na kwa wale wote ambao kwa namna moja ama nyingine, na kwa kujitoa kwao kumefanikisha kusainiwa leo kwa mikataba hii. Kwa namna ya kipee, niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Burundi kwa utayari wake wa kutekeleza mradi huu wa barabara ya Kikanda, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Wakala wa Uwezeshaji

wa Usafiri wa Kanda ya Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency) kwa kujitoa katika kufanikisha mchakato huu. Ni matumaini yangu kwamba moyo huu wa kujitolea kwa juhudi na maarifa utaendelezwa katika kufanikisha utekelezaji wa mradi huu.

- 6. Ndugu Mwakilishi Mkazi, Mabibi na Mabwana,** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu sana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuzidi kuimarisha na kuboresha ushirikiano uliopo kwa maendeleo endelevu ya wananchi wa Tanzania. Aidha, Serikali itachukua kila hatua inayotakikana katika utekelezaji wa miradi huu ili kuweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Ahsanteni kwa Kunisilikiza**